

NDIPO YESU AKAJA NA KUITA



Yohana Mtakatifu, mlango wa 11, kuanzia kifunga cha 18, ninataka kusoma.

Na Bethania ilikuwa karibu na Yerusalemu, kadiri ya maili mbili hivi;

Na watu wengi katika Wayahudi walikuwa wamekuja kwa Martha na Mariamu, ili kuwafariji kwa habari ya ndugu yao.

Basi Martha aliposikia kwamba Yesu anakuja, alikwenda kumlaki; na Mariamu alikuwa akikaa nyumbani.

Basi Martha akamwambia Yesu, Bwana, kama ungalikuwapo hapa, ndugu yangu hangalikufa.

Lakini hata sasa najua ya kuwa yo yote utakayomwomba Mungu, Mungu atakupa.

Yesu akamwambia, Ndugu yako atafufuka.

Martha akamwambia, Najua ya kuwa atafufuka katika ufufuo siku ya mwisho.

Yesu akamwambia, Mimi ndimi huo ufufuo, na... uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi;

Naye kila aishiye na kuniadini hatakuwa kabisa hata milele. Je! Unayasadiki hayo?

Akamwambia, Naam, Bwana, mimi nimesadiki ya kwamba wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu, yule ajaye ulimwenguni. (Hebu angalia jambo hilo!)

Naye alipokwisha kusema hayo, alikwenda zake; akamwita umbu lake Mariamu faraghani, akisema, Mwalimu yupo anakuwa.

² Na tuombe. Baba wa Mbinguni, thibitisha Maneno hayo mioyoni mwetu, usiku wa leo, tunapokungojea Wewe sasa. Neno Lako, mtumishi Wako, na maandiko haya, yote yamesalimishwa Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mnaweza kuketi.

³ Kusudi langu la kuwa hapa ni kujaribu kuwasaidia watu wa Mungu. Si sana sana kuomba, na kuwawekea mikono wagonjwa, bali kwamba wantambue Yesu Kristo miongoni mwetu, Mwana wa Mungu miongoni mwetu. Tunazungumza usiku wa leo juu ya somo hili: *Ndipo Yesu Akaia na Kuita.*

⁴ Sasa katika wakati huu tunaozungumza habari zake, ulikuwa ni wakati wa huzuni sana. Kama ulipata kusoma

hadithi hiyo katika maisha ya Bwana wetu, tunaona ya kwamba Yeye alikuwa rafiki mpenzi wa mvulana huyu, Lazaro. Alikuwa . . . Baada ya Yusufu kuaga dunia, ama alikuwa ameondoka na akaja kuishi na Martha, Mariamu, na Lazaro. Nao walikuwa marafiki wapenzi. Walikuwa . . . Yeye alikuwa ni kama mchungaji kwao, rafiki ha—halisi. Nao walimshonea vitu vidogo vya kuvaa, kabuti la kuvaa, ninaamini, wanadai, na lilikuwa limefumwa lote bila upindo. Na halafu walikuwa wamemtendea vitu fulani fulani, kwa sababu walimwamini. Ilikuwa wao—wao walikuwa wameamini na walikuwa wameona jambo hilo. Walikuwa wameondoka kanisani, na kadhalika, wapate kumfuata. Na hilo lilikuwa ni jambo kubwa katika siku ile, ambalo hata adhabu yake ingeweza kuwa ni kifo, ku—kuliacha.

⁵ Lakini, Yesu, Jamaa huyu aliyekuwa akizunguka huku na huko jinsi walivyodai, akiyararua makanisa yao, na kusema jambo ovu kuhusu kuhani wao, na—na kadhalika, Yeye alikuwa—Yeye alikuwa amewatendea madhara makubwa, ndivyo walivyodhani. Na—na hata kumkiri ingekuwa ni ku—kutupwa nje ya masinagogi. Na basi kama ukiwa nje ya kanisa, wali—walidhani hukuwa na—na nafasi ya kupata ukombozi. Kama hukuwa mfuasi wa moja ya madhehebu yao, kama vile Farisayo, Sadukayo, ama kitu fulani, ilikuwa hakuna ukombozi kama ulikuwa nje ya hayo. Na kama wao walikuwa na haki, funguo, pia wangekufukuza tu kama wangetaka. Hilo lilikuwa ndilo tamshi lao wenyewe. Si ajabu Yesu alisema, “Ninyi, kwa mapokeo yenu, mmelitangua Neno la Mungu.” Mnaona?

⁶ Na sasa hilo jambo limejirudia tena, maana sote tunajua historia hujirudia kila kipindi fulani. Na ni jambo la huzuni kulisema, bali ilitabiriwa kujirudia, na imefanya hivyo tena.

Tunaona ya kwamba Yesu hakuwaziwa mema.

⁷ Mara nyingi, watu hupenda kumhukumu mtu asiye kubaliana nao. Hatupaswi kufanya hivyo. Tunaweza tusikubaliane sisi kwa sisi, lakini tuwe marafiki. Kama nisingeweza kutokubaliana na mtu fulani, na bado nimpende na kumwombea, na kutokubaliana naye juu ya msingi wa Maandiko, na kwa sababu ya mwangaza bora zaidi, basi sitasema kitu chochote juu ya mtu huyo. Daima ninataka kutokubaliana naye, kwa namna ya kirafiki, maana ninampenda, na hakika si—sitaki yeye apotee. Naye anapaswa kufanya jambo lilo hilo kwangu mimi; hatutaki kupotea. Nasi inatupasa kuweka mawazo yetu kwenye msingi wa yale Neno lisemayo. Neno na liwe ndiyo Kweli. Si kanuni yetu ya imani wala vile mawazo yetu yalivyo, bali yale Yeye asemayo; hakuna kujifasiria kama apendavyo mtu yeyote, ni vile tu Neno lilivyosema.

⁸ Hivi majuzi usiku, nilifanya jambo fulani nalo lilionekana karibu ni la kukufuru, ninaamini ilikuwa ni kwenye kiamshakinywa cha wahudumu hivi majuzi asubuhi. Nilimweka Yesu mahakamani. Nilisema, “Kama tu walivyofanya wakati huo, ndivyo wafanyavyo leo.” Labda lingekuwa ni jambo linalofaa kama nikilirudia kwa muda mfupi tu, ikiwa tuna wakati. Sasa, nilisema, leo tunaona ya kwamba . . .

⁹ Katika matengenezo ya Luther, yeye, katika wakati huo, yeye alisema wenye haki wataishi kwa imani. “Mtu aminiye, ndiye aliyempata.” Lakini tuliona ya kwamba wengi wao walisema waliamini, wala hawakumpata.

¹⁰ Katika siku za—za John Wesley, kama watu walipata baraka ya pili, waliita utakaso, utakaso mzima, walijawa na furaha wakupaza sauti. “Kila mtu aliyepaza sauti, alikuwa Nae.” Bali walikuta ya kwamba hawakumpata. Wengi wao walipaza sauti, wala hawakumpata.

¹¹ Siku za Pentekoste, walisema, “Sasa kule kurudishwa kwa vipawa kumekuja, ule ubatizo wa Roho Mtakatifu. Yeye anenaye kwa lugha, amempata.” Tunaona ya kwamba wengi walinena kwa lugha, wala hawakumpata.

¹² Kwa hiyo wao wanasema, “Vema, tunda la Roho, huyo alikuwa Ndiye.” Loo, la, si tunda la Roho. Wakristo wa Kisayansi wanalo hilo, ambapo hata ni vigumu kwao . . . Upendo ni tunda la Roho. Halafu, nao wana upendo mwingi zaidi kuliko mtu mwingine yeyote, na wanakana Uungu wa Yesu Kristo; wanamwita tu nabii fulani hivi, mtu wa kawaida tu. Unaona? Kwa hiyo hilo silo linalotenda jambo hilo.

¹³ Hebu niulize swali juu ya jambo hilo kidogo. Hebu na tumpandishe Yesu kizimbani. Na Mungu na anisamehe kwa tamshi hili, kutoka hapa jukwaani, bali nitasimama dhidi Yake kwa kitambo kidogo, kusudi tu niwalettee Nuru. Unaona?

¹⁴ “Sasa nina ninyi watu hapa usiku wa leo; ninazungumza na ninyi. Nilikuwa nimerudi huko nyuma zamani ambapo Yesu wa Nazareti alikuwa hapa duniani. Ninakuja kwenu, na kujenga hoja nanyi dhidi ya Jamaa huyu, Yesu wa Nazareti. Sasa sote tunajua ya kwamba Mungu ni upendo. Biblia inasema Yeye ni upendo. Vema, na upendo, Roho ni uvu- . . . uvumilivu, utu wema, subira, upole, na kadhalika, na upendo. Sasa ningesema, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Tutachukua yale—yale tujuayo, Mkristo alivyo.

¹⁵ “Hebu mwangalieni maskini huyu kuhani wenu. Babu wa babu wa babu yake alikuwa kuhani. Ilibidi azaliwe kwenye ukoo huo wa Walawi, kuwa kuhani. Tunaona, sasa, yeye hana maisha ya ujana kama wengine wenu mlivyokuwa nayo. Yeye anafanya nini? Yeye hujitolea, yeye yuko huko apate kusoma Neno, Neno la Mungu. Analisoma, usiku na mchana, usiku na mchana, inambidi kujua kila herufi yake, kila neno katika

gombo. Inambidi kulijua kwa moyo. Yeye—yeye, kitu fulani tu juu ya jambo hilo ambacho anapaswa kujua.

¹⁶ “Ndipo, licha ya hayo, wakati baba yako na mama yako walipofunga ndoa, ni nani aliyewaunganisha pamoja kama mume na mke? Maskini kuhani wenu mcha Mungu. Ni nani aliyekuja kwa baba yako wakati alipokuwa na hitaji na aliwiwa pesa shambani mwake, ambalo lilikuwa lichukuliwe na waweka rehani. Ni nani aliyemtetea? Maskini kasisi wako mwema. Ni nani aliyemsaidia mama yako kwenye kile chumba wakati alipokuwa akikuzaa? Maskini kasisi wako mwema. Ni nani anayekuja kwako wakati ukiwa mgonjwa na mhitaji? Maskini kasisi wako mwema. Ni nani aliyekubariki na kukukabidhi kwa Mungu, na kukutahiri kwenye siku ya nane? Maskini kasisi wako mwema. Wakati baba yako na mama walikuwa karibu kutalikiana, ni nani aliyewapatanisha, akawafanya waridhiane? Maskini kasisi wako mwema. Shida inapotokea ujirani, ni nani anayeishughulikia? Maskini kasisi wako mwema. Hakika.

¹⁷ “Sasa Maskini kuhani huyu mwema anajua ya kwamba Biblia ilisema ya kwamba Mungu anahitaji mwana-kondoo kwa ajili ya sadaka. Wengi wenu ninyi wanaume ni wafanyabiashara, kwa hiyo hamfugi kondoo, hata hivyo Mungu anataka kondoo. Walitengeneza vibanda kadhaa kule, waliuza kondoo wao ili kwamba wa—wafanyabiashara wangeweza kwenda kule na kuwanunua, wakitoa dhabihu kwa ajili ya nafsi zao, dhabihu ambazo Mungu ndizo anazotaka.

¹⁸ “Je! huyu Kijana, anayelitwa Yesu, ni kitu gani alifanya? Yeye alitoka wapi? Inasemekana alizaliwa, uzao mtakatifu wa bikira. Ni nani aliyepata kusikia upuuzi kama huo? Tunajua ya kwamba mama yake alimzaa kabla Yeye na Yusufu hawajazaliwa... ama yeye na Yusufu hawajafunga ndoa, Yeye alizaliwa. Sasa tunaona ya kwamba Yeye ana ninii—Yeye ana sifa mbaya, kwanza.

¹⁹ “Yeye ana kitambulisho gani cha ushirika? Kama alikuwa mcha Mungu, je! alijiunga na kundi gani? Wakati ambapo kuhani wenu alisoma, akasoma, akasoma, akasoma, apate kulijua hilo Neno; Huyu hapa anakuja, akibomoa yale aliyojenga. Je! hivi ungeweza kuita kitu hicho kwamba ni ‘Mungu’? La hashu.

²⁰ “Sasa, hivi majuzi, wakati kuhani wenu alipokuwa amepatengeneza mahali pale kule juu, ninii...na ndipo mahali ambapo mngeweza kununulia sadaka, hivi huyu kijana alifanya kitu gani? Ati wema? Aliwapiga, alisokota kamba, baadhi ya...?...na akawaangalia hao watu, kwa hasira, akaziangusha hizo meza, na kuwapiga akawafukuza watoke hapo. Nawe unaita jambo hilo ni matunda ya Roho, ati kuwaangalia watu, kwa hasira? Na, hebu angalia, kumnyima mtu fursa yake ya kumwabudu Yehova! Mfanyabiashara anataka kumwabudu Mungu; mfanyabiashara hafugi wana-

kondoo, naye alitoka akaenda kule kuwanunua. Na Yeye akazipindua, na kuwafukuza, na kuwatoa nje.”

²¹ Ni nani aliye na tunda la Roho hapo? Mnaona? Hilo hapo. Unaona, si tunda la Roho, si kunena kwa lugha, si kupiga makelele.

²² Unasema, “Basi, Ndugu Branham, ushahidi ni nini? Ushahidi ni nini?” Ni uthibitisho wa Neno la wakati.

²³ Walikuwa na Biblia. Yeye alikuwa barabara kabisa vile Yehova alivyosema ingetukia. Halihitaji fasiri yoyote. Limefasiriwa pale. Hao hapo makuhani wako, hayo hapo yote waliyokuwa nayo, na chochote kile kimeyekwa tu katika kawaida ya kila siku na kila kitu, bali hata hivyo walishindwa kuliona Neno. Naye alilifanya Neno hilo hai kwa ajili ya wakati huo. Huo ndio ushahidi wa wakati huo.

²⁴ Luther alikuwa na ushahidi wa kipindi chake, Wesley wa wakati wake, Pentekoste wa wakati wake, bali sisi tuko katika wakati mwingine. Mambo hayo ni mazuri. Lakini kama vile mtoto mchanga, alivyo na kidole, jicho, na pua, lakini baada ya kitambo kidogo hana budi kufanyika binadamu. Hana budi kufanyika mtoto m—mzima; kisha azaliwe, awe na nafsi, mwili, roho, anaweza kwenda huku na huko.

²⁵ Sasa tunaona ya kwamba, yote haya, Yesu alikuwa ameyatangaza kwa watu wachache tu. Wale tu aliokuwa amewakusudia Uzima, walimwona Yeye. Si umati mkubwa; umati wake usingeweza kuwa kama umati wa Kayafa. Mbona, Kayafa angaliweza kulikusanya taifa zima pamoja. Yesu aliwakusanya watu wachache tu pamoja. Si wengi waliomjua. Maelfu mara maelfu, wakati yeye alipokuja duniani. Alipita duniani, wala hata hawakujua yeye alikuwa hapa.

²⁶ Ndivyo walivyofanya tena! Yeye atawajia wale walioitiwa Uzima. Yeye anajua ni nani aliyeitiwa Uzima. Wala hataninii . . . Ni kazi Yake kushughulikia jambo hilo.

²⁷ Sasa tunaona hilo basi walitoka kanisani, nao walikuwa wamemwamini. Kila kitu Neno lilichokuwa likisema kumhusu Yeye, Huyu hapo.

²⁸ Na siku moja aliondoka nyumbani mwao. Ninataka kuzungumza juu ya mambo matatu: Yesu alikuwa ameondoka; mauti ilikuwa imekuja; na matumaini yote yalikuwa yamekwisha. Ninataka kuzungumzia mambo hayo matatu kwa dakika chache.

²⁹ Yesu alikuwa ameondoka. Na wakati alipoondoka, shida ikaingia. Sasa wakati anapokuacha, ama kuacha nyumba yako unayokaa, shida iko njiani. Shetani ana mlango wazi wakati Yesu anapoondoka.

³⁰ Alikuwa amekwenda zake, na—na mara alipoondoka, basi mauti ikaingia. Na wakati Yesu anapotoka, mauti huingia.

Kutengwa Naye ni mauti, kwa hiyo mauti iliingia wakati Yesu alipotoka.

³¹ Na mauti ilikuwa imedumu kitambo na Lazaro. Na ndipo Yule waliyekuwa wamemwamini na kumpenda, walikuwa wametuma aje amwombe Lazaro, maana walikuwa wamemwona na wakajua ya kwamba Yeye alimjua Mungu, kwamba lolote ambalo Mungu... Martha alisema jambo hilo kule nyuma, "Lolote utakalomwambia Mungu sasa, Mungu atalifanya." Alitambua ya kwamba Yeye na Mungu walikuwa mmoja. Yeye alikuwa ndilo Neno la saa hiyo, kwa hiyo alitambua jambo hilo. Naye alijua, kama angaliweza tu kuwasiliana Naye, bali alikuwa ameondoka wala hawakuweza kumpata. Nao wakaagiza aje, na, badala ya Yeye kuja, alizidi kwenda mbali zaidi. Na basi wakamwagiza tena, na, badala ya Yeye kuja, akaenda mbali zaidi.

³² Wakati mwingine hatujui kwa nini mambo hayo hutendeka, lakini hivi Maandiko hayasemi ya kwamba "Mambo yote hutenda kazi kwa manufaa ya wale wanaompenda Mungu"? Yeye anajua analofanya. Kama akichelewa, hilo ni sawa. Yeye anajua anachofanya. Kulikuwa na kusudi fulani.

³³ Tunaona ya kwamba Yeye alisema, katika Yohana Mtakatifu 5:19, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kufanya kitu kwa nafsi Yake, bali yale anayomwona Baba akitenda."

³⁴ Baba alikuwa amemwambia aondoke zake, na aondoke zake kwa siku kadhaa. Baada ya siku hizo kutimia, ndipo akasema aliyosema basi, ya kwamba, "Rafiki yetu Lazaro analala."

Ndipo mmoja akasema, "Vema, anafanya vema."

³⁵ Yeye akasema, "Amekufa. Na kwa ajili yenu nina furahi sikuwako." Maana, wangukuwa wakifanya bidii kumfanya aende kwake, kumponya ama kusema kile kilichopaswa kufanywa. Bali Yeye alijua yale yaliyopaswa kufanywa, kwa hiyo alikuwa amefanya vile vile hasa alivyokusudiwa kufanya; kuondoka. Mnamwona pale kaburini wakati aliporudi. Alisema jambo hilo wakati aliporudi na kuyaona makazi haya.

³⁶ Matumaini yote yalikuwa yamekwisha. Lazaro alikuwa amekufa. Kila saa, walikaa kuwazia, "Huenda akatokea. Huenda akatokea. Huenda akarudi." Hatimaye, akafa, pumzi ikamwacha.

³⁷ Wakatoka, wakamtia dawa asioze, wakiitoa damu kutoka mwilini mwake, wakamfunga kwa kitani, viungo, na wakamtia dawa asioze na wakamlaza kaburini, wakafunika kaburi hilo kwa jiwe, jambo ambalo lilikuwa ni desturi yao ya kuzika katika siku hizo. Shimo sakafuni, labda tu mwambani, na kulifunika kwa jiwe, hiyo ilikuwa ndiyo desturi yao.

³⁸ Siku ya kwanza ikapita, siku ya pili ikapita, siku ya tatu ikapita, siku ya nne ikapita, mtu huyo alikuwa tayari anaozea

kaburini. Pua yake labda ilikuwa imedidimia. Hiyo, nafikiri hicho ndicho kitu cha kwanza kinachodidimia, ni pua. Naye alikuwa tayari ameoza. Mwi—mwili wake ulikuwa umeyarudia mavumbi, ya ardhi, ama ulikuwa ukiyarudia. Nafsi yake ilikuwa imesafiri kwa muda wa siku nne mahali fulani, kutoka kwake.

³⁹ Matumaini yote ya kupata kumwona tena, katika maisha haya, yalikuwa yameondoka. Na ndipo wakati matumaini yote yalipokuwa yamekwisha... Walikuwa wamengojea, “Labda kama atakuja siku ya kwanza, siku ya pili!” La. Ndipo akafa, wala hakuwa amekuja. Ndipo kukata tamaa kukaingia.

⁴⁰ Baada ya kitambo kidogo kulikuwa na mtu ambaye hapana budi alikuwa amemwambia, “Bwana yuko nje.” Huyu hapa Martha akishuka kwenda barabarani!

⁴¹ Yesu alikuja katika saa hiyo yenye giza wakati kila tumaini lilikuwa limekwisha. Huo ndio wakati Yeye anapokuja kwa kawaida. Unaona? Yeye huja tu katika wakati huo wenye giza totoro, ndipo Yesu anapojitokeza jukwaani.

⁴² Sasa angalia, Yeye alikuja na akamwita Martha. Uwepo Wake ulileta matumaini mapya. Haidhuru kama mvulana huyo alikuwa amekufa, hata hivyo Uwepo Wake huleta tumaini jipya.

⁴³ Huenda ukawa umeketi hapa usiku wa leo, rafiki yangu, ambapo madaktari wamekukatia tamaa, kwa kansa, ugonjwa wa moyo. Labda katika kiti cha magurudumu, u kiwete, sayansi yote imesema hakuna matumaini kwako; kulundikana kwa madini ya kalisi kume-kumetia mifupa ya—ya—yako vifundo, hivi kwamba huwezi kuikunja tena. Ama, aidha moyo wa—wako una hali mbaya sana, daktari anasema huenda ukaondoka dakika yoyote. Loo, na ni kundi kubwa la watu wenye kansa na TB, labda ndilo tumaini la mwisho ulilo nalo, na inaonekana kana kwamba daktari amekukataa. Hata hivyo, kuwa kwenye ule Uwepo na kutambua Uwepo wa Yesu Kristo, huleta matumaini tena.

⁴⁴ Mtu fulani anaweza hata kukutajia jambo hilo. Labda hujapata kulisikia hapo kabla, bali hebu mtu fulani aseme, “Ninajua mahali palipo na kanisa, wanamwamini Mungu na wanawaomba wagonjwa,” upesi sasa (unakaribia kufa), unaona, matumaini mapya yanazuka. Daima huzuka. Katika hiyo saa yenye giza, hapo ndipo kwa kawaida mtu fulani husema jambo fulani juu ya jambo hilo, anakwambia juu ya Yesu. Uwepo Wake ulileta matumaini mapya.

⁴⁵ Jalia Huo ufanye jambo lile lile usiku wa leo, kama ulivyofanya jana usiku, wakati tunapona lile Neno lililothibitishwa pasipo uvuli wowote wa tashwishi, ambalo limedhihirishwa na kuthibitishwa; ya kwamba Yesu yule aliyeishi miaka elfu moja mia tisa iliyopita, ambaye alikufa pale Kalvari, alifufuka siku ya tatu, na akawatokea wale wanafunzi na kuyafumbua macho yao, na kufanya ahadi hii ya siku hii,

yupo papa hapa leo mbele zetu sasa usiku wa leo. Halina budi kuleta matumaini kwa watu. Matumaini mapya yatokea ghafla.

⁴⁶ Labda mtu fulani alisema, “Kanisa kwa namna fulani limekauka kwa muda kidogo. Hatujawahi kuwa na maji yoyote safi kwa—kwa—kwa miezi michache. Hatujakuwa na uamsho. Inaonekana kana kwamba kila mtu amekwama, ama kitu kama hicho. Tunaenda tu kanisani na kuimba wimbo, na—na kusikia jumbe chache na kurudi.” Lakini mara, basi, tunapoanza kukauka, ndipo Yesu anajitokeza jukwaani, anatuburudisha, hutuletea jambo fulani jipya. Yeye daima yupo hapo kufanya jambo hilo. Matumaini mapya huja wakati—wakati Yesu anapointia. Uwepo Wake husababisha tumaini jipya.

⁴⁷ Yeye alijua ya kwamba Yeye alikuwa ndiye lile Neno la Mungu lililodhihirishwa. Alikuwa ameuona wakati huo. Ama, kama asingeuona, angali angekuwa bado yuko kwenye Orthodoksi. Angalikuwa bado ni mfuasi wa kanisa. Bali alikuwa ameona hilo Neno lililoahidiwa. Alikuwa ameona hilo Neno lililoahidiwa likidhihirishwa na Yeye na alijua ya kwamba Yeye alikuwa ni lile Neno lililo hai. Ndipo wakati aliposikia habari hiyo, hakujali ni wangapi waliompinga, chochote kile, alimkimbilia upesi alivyoweza. Unaona? Yeye alijua alikuwa Ndiye lile Neno lililodhihirishwa.

⁴⁸ Hapana shaka ila kile alichokuwa amesoma juu ya hadithi ya Eliya katika siku yake. Sasa, yeye alikuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa katika siku hiyo. Alikuwa nabii, na Neno la Bwana humjia nabii. Na kulikuwa na mwanamke pale ndani, aliyekuwa na mtoto mchanga aliyekuwa amepewa kwa baraka ambayo nabii huyo alikuwa amembariki kwayo, naye alimpata mtoto huyo.

⁴⁹ Siku moja, yapata saa tano, hapana budi alipatwa na ugonjwa wa jua kali. Alikuwa huko nje kondeni pamoja na baba yake, Biblia haisemi ilikuwa ni ugonjwa huo, tuseme ilikuwa ni ugonjwa wa kupatwa na jua kali, bali alianza kulia, “Kichwa changu! Kichwa changu!” Yapata saa tano mchana. Naye alimwagiza mtumishi, baba alimwagiza, ampeleke nyumbani. Alilazwa kwenye paja la mama yake mpaka karibu na alasiri, akazidi kuwa mgonjwa zaidi na zaidi, na hatimaye akafa.

⁵⁰ Na sasa, badala ya kukata tamaa, majirani wote walikuja wakilia kwa sauti kuu na kupiga makelele. Lakini yule mama imara, mtoto wake mchanga alikuwa amekufa, alimchukua akamwingiza kwenye kile chumba kidogo alichokuwa amemwandalia yule nabii, na akamlaza kitandani mwake, namna hiyo. Ndipo akamwambia yule mtumishi, “Nitandikie nyumbu, na umwendeshe moja kwa moja, wala usisimame isipokuwa nikwambie.” Loo, jamani! Jambo ndilo hilo!

⁵¹ Hatuna wakati wa kujadiliana na kuzozana. Haya yamepitwa na wakati. Hebu na tusonge mbele. Inatupasa kufika kule. Tuna haja.

⁵² Na kwa hiyo yeye akasema, “Songa mbele, wala usilegeze mwendo wako isipokuwa nikuamuru.” Ndipo wakaenda mpaka wakamfikia Eliya.

⁵³ Eliya, akiwa ni mtu wa Mungu, si kama Kristo; Kristo alijua mambo yote, maana Yeye alikuwa Mungu. Eliya alikuwa sehemu ya Mungu. Huyu alikuwa ni Kristo katika Eliya. Na huo ulikuwa ndio ujumbe wa wakati huo, kwa maana Neno la Bwana kwa ajili ya wakati huo lilikuwa lina nabii huyo.

⁵⁴ Yesu alikuwa ni utimilifu wa manabii hao wote, kila mmoja wao alimdhahirisha tu Yeye. Hivyo tu. Tokea mwanzo tangu kwa Yusufu, toka kwenye vile vipande thelathini vya fedha, kila mahali, Yeye—Yeye alimwonyesha Kristo. Vivyo hivyo na Musa pia!

⁵⁵ Daudi, akiketi kama mfalme aliyekataliwa juu ya kile kilima, akilia kwa sababu alikuwa amekataliwa. Miaka mia nane baada ya jambo hilo, Mwana wa Daudi aliketi juu ya kilima. Huyu alikuwa ni Roho wa Kristo katika Daudi pale. Naye...Jamani! Yeye alikuwa Shina na Mzao wa Daudi pia. Na kwa hiyo aliketi juu ya kilima, akilia, kama Mfalme aliyekataliwa, “Yerusalem, Yerusalem, ni mara ngapi ningalikufunika, kama kuku avifunikavyo vifaranga vyake.” Ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni Kristo kule nyuma.

⁵⁶ Ilikuwa ni Kristo akilia wakati Daudi alipoandika ule wimbo, “Mungu Wangu, mbona umeniacha. Mifupa yangu yote, inanikodolea macho. Waliichoma miguu Yangu na mikono Yangu. Waligawanya mavazi Yangu miongoni mwao. Walipigia kura vazi langu.” Huyu alikuwa ni Kristo akinena katika Daudi. Hiyo ni kweli. Yeye alikuwa ni onyesho la Neno. Kristo alikuja kutimiza yale mambo ambayo yalikuwa yamenenwa na manabii, maana Neno lilikuwa na manabii.

⁵⁷ Yeye alisema jambo hilo katika lile somo jana usiku, ya kwamba alikuja kutimiza yale manabii waliyokuwa wamesema juu Yake, maana wao walikuwa na Neno. Na Eliya alikuwa nabii wa Mungu, Neno la siku hiyo.

⁵⁸ Kwa hiyo mwanamke huyo Mshunami alikaa na nabii huyo mpaka akaja na kudhihirisha nguvu za Mungu, na akajilaza juu ya mtoto huyo mchanga, ndipo mtoto huyo mchanga akafufuka.

⁵⁹ Sasa hapana budi Martha alitambua jambo hili, ingawa alikuwa na shughuli nyingi akishughulikia mambo ya nyumbani, akiosha vyombo, na kadhalika. Lakini pale alionyesha jinsi alivyo. Alionyesha hasa kile kilichokuwa ndani yake. Alienda kumleta mara moja. Kama Mungu alikuwa ndani ya Eliya, ilibidi Mungu awe katika Kristo, maana alikuwa amethibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye yule Mtu. Amina. Ninapenda

jambo hilo, ushupavu huo! Anamwendea. Ilimbidi kumleta. Naye akakuta kwamba kule, alipofika Kwake—Kwake; sasa kumbukeni, alijua ya kwamba kamwe habadilika, ya kwamba Mungu kamwe habadilishi mpango Wake. Kama alikuwa katika Eliya na angeweza kufufua wafu, Yeye alikuwa katika Kristo na angeweza kufufua wafu, ingawa hakuwa amefanya hivyo, maana ni Mungu yeye yule.

⁶⁰ Wala Yeye habadilika bado! Ni Mungu mwenye uwezo mkubwa tu usiku wa leo kama alivyopata kuwa. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye habadiliki.

⁶¹ Na Yeye alijua ya kwamba mama huyo alijua jambo hilo lilikuwa ndani Yake. Angalia, katika dakika chache tu ilithibitisha jambo hilo, wakati alipomwambia jambo fulani kuhusu ndugu yake, naye akasema, “Bwana, ni—ninaamini ya kwamba Wewe Ndiye.”

⁶² Naye akasema, “Mimi Ndimi huo Ufufuo na Uzima. Mtu ajapokufa, atakuwa anaishi. Na yeye aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. MIMI NDIYE.” Huyu ni yule MIMI NIKO aliyekuwa katika kijiti kilichowaka moto, pamoja na Musa. “Mimi Ndimi huo Ufufuo. Mimi Ndimi Uzima. Nilikuwa ndiye ule ukuta. Ningali Yeye. Mimi Ndimi Ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo atakuwa anaishi. Yeye aliyehai na kuniamini Mimi, hatakufa kamwe.” Baada ya hakikisho hili kuu alilokuwa nalo, ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Neno lililoahidiwa; wakati Yeye aliposema, akiwa ni Nabii, asingeweza kusema uongo; kwa hiyo Yeye, wakati aliposema, “Mimi Ndimi AMBAYE NIKO. Mimi Ndimi huo Ufufuo na Uzima.”

⁶³ Akasema, “Ninaamini ya kwamba Wewe Ndiye, Mwana wa Mungu yule ajaye ulimwenguni. Ingawa ndugu yangu amekufa, amelala kule nje kaburini, yeye...mwili wake unaoza sasa; lakini hata sasa, lolote usemalo, litatimia.” Kweli!

⁶⁴ Yote aliyotaka ilikuwa ni kumsikia Yeye akisema jambo hilo! Amina. Loo, Martha, tuko wapi usiku wa leo? “Sema tu Neno; mtumishi wangu ataishi!” kumsikia tu akisema jambo hilo! Huenda walikuja wakamwambia ya kwamba Yeye alisema jambo hilo, bali huyu hapa Yeye Mwenyewe. Ee Mungu, yafungue macho yaliyopofushwa, kusudi yapate kuona! Wakati Yeye, katika Uwepo Wake, anaposema Neno, daima linadhihirishwa.

⁶⁵ Akasema, “Lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupata. Hebu tu nijalie nisikie!” Alimtaka aseme Neno. Hilo tu ndilo alilotaka kusikia. Kupata tu Neno, hilo tu ndilo alilohitaji, ilikuwa ni kumsikia Yeye akisema angefanya hivyo.

⁶⁶ Naye angalifanya jambo hilo papo hapo, lakini, unaona, kwa ono ambalo Baba alikuwa amemwonyesha, ilimbidi Yeye awe amesimama karibu na lile kaburi. Loo, jamani! Shikilieni imani

yenu! Mungu anatenda kila kitu sawasawa. Itakuwa sawa. Ngoja tu mpaka yule mama alipofika kaburini.

⁶⁷ Angalia, Martha angefanya tu Yesu kusema jambo hilo, hata wakati yeye alikuwa bado... Matumaini yote yalikuwa yamekwisha, kila kitu. Alikuwa amekufa, akioza kaburini, bali kumsikia tu akisema jambo hilo, ndilo tu alilotaka huyo mama.

⁶⁸ Sasa wakati aliposema, "Mimi Ndimi Ufufuo na Uzima," aliamini jambo hilo. Aliliamini. Sasa angalia, sasa ilimbidi kuamini yasiyowezekana, wakati alipomsikia akisema, "Mimi Ndimi huo Ufufuo na Uzima. Mtu ajapokufa, atakuwa anaishi, naye kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kabisa." Kasema, "Je! unayasadiki hayo?"

⁶⁹ Naye akasema, "Naam, Bwana, nimesadiki. Nimesadiki ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu yule ajaye ulimwenguni." Ninapenda jambo hilo. Ninapenda jambo hilo.

⁷⁰ Nimesema jambo hilo hapo kabla. Huenda likawekwa tena sasa. Nilikuwa nikizungumza na mwanamke mmoja si muda mrefu uliopita, ilikuwa ni kanisa fulani nililotaja muda mfupi uliopita, ambalo haliamini ya kwamba Yeye alikuwa Mungu, Uungu Wake; alikuwa nabii tu, mtu tu wa kawaida.

⁷¹ Yeye alikuwa hivyo, kweli. Yeye alikuwa hivyo, pamoja na kuwa Mungu. Unaona, Yeye alikuwa dhihirisho. Yesu ni ule mwili, yule Mvulana, yule Mtu; Mungu alikuwa ni kile kilichoishi ndani Yake. Mungu alikuwa ndani Yake. Yeye alikuwa ni Mungu-mwanadamu. Alikuwa Mwanadamu, hata hivyo alikuwa ni Mungu aliye dhihirishwa katika mwili. Tunapomwona Yesu, tunamwona Mungu. Hivyo ndivyo Yeye alivyosema, "Unapomwona Baba, unaponiona Mimi, unamwona Baba." Kwa sababu, Yeye alikuwa ni uakisi, kwa maana alikuwa ni Neno, amina, lililokuwa hapo mwanzo. Amina.

⁷² Yeye alikuwa amewaita manabii, "Mungu." Je! unajua jambo hilo? Yeye alisema, "Mnawaita 'Mungu' hao ambao Neno la Mungu linawajia. Mnawezaje kunihukumu ninaposema, 'Mimi ni Mwana wa Mungu'?"

⁷³ Maana, Neno lile lile lilisema Yeye angekuwako, na hilo hapo Neno lililodhihirishwa tena. Na hata hivyo wasingeamini jambo hilo.

⁷⁴ Mwanamke huyu aliniambia, "Ninaweza kukuthibitishia." Kasema, "Ninapenda kukusikia ukihubiri, bali kuna jambo moja unalofanya kupita kiasi."

"Vema, ni lipi hilo?"

Kasema, "Unajivuna kupita kiasi juu ya Yesu."

⁷⁵ Nikasema, "Ninatumaini ya kwamba hilo tu ndilo Yeye alilo nalo dhidi yangu atakapokuja." Naye akasema... Nikasema, "Ninatumaini hilo tu ndilo awezalo, kosa analoweza kulipata kwangu." Nikasema, "Kama ningalikuwa na ndimi elfu kumi,

nisingeweza kuzungumza vya kutosha, loo jamani, kile alichu Yeye!”

Akasema, “Lakini, wewe, wewe unamfanya Yeye kuwa Mungu.”

⁷⁶ Nikasema, “Alikuwa. Au, kama hakuwa, Yeye alikuwa ni mdanganyifu mkubwa kabisa ulimwengu uliwahi kuwa naye.”

Akasema, “Yeye alikuwa nabii.”

⁷⁷ Nikasema, “Yeye alikuwa nabii, hiyo ni kweli: Mungu-nabii, utimilifu wa Neno. Nabii alijiliwa tu na Neno, hilo ndilo linalomfanya—lililomfanya nabii. Bali Yeye alikuwa utimilifu wa hilo Neno.”

⁷⁸ Naye akasema, “Ninaweza kukuthibitishia.” Kasema, “Unamfanya kuwa Mungu.”

Nikasema, “Yeye alikuwa Mungu.”

Naye akasema, “Hawezi kuwa Mungu.”

Nikasema, “Lakini alikuwa hivyo.”

Akasema, “Ulisema uliamini Biblia.”

Nikasema, “Ninaiamini.”

⁷⁹ Akasema, “Nitakuthibitishia, kwa Biblia yako mwenyewe, ya kwamba Yeye hakuwa Mungu.”

⁸⁰ Nikasema, “Thibitisha. Kama Biblia inasema hivyo, basi nitaamini, maana ninaamini Neno liko sahihi.”

⁸¹ Akasema, “Kule barabarani akitoka kwenye kaburi la Lazaro, je! unakumbuka jambo hilo katika Yohana Mtakatifu 11?”

Nikasema, “Hakika ninakumbuka, mama.”

⁸² Kasema, “Vema, sasa, alipokuwa kule barabarani, Yeye alilia. Biblia ilisema, “Alilia.”

Nikasema, “Hakika, Biblia ilisema alilia.”

Kasema, “Je! angeweza kuwa Mungu na alie?”

Nikasema, “Yeye alikuwa mwanadamu.”

“Mwanadamu na Mungu?”

⁸³ Nikasema, “Naam, bibi. Unashindwa kuona. Alikuwa mwa—mwanadamu akishuka kwenda kule, akilia pamoja na wale waliokuwa wakilia, hiyo ni kweli, akihuzunika pamoja na wale waliohuzunika. Yeye alikuwa Mwanadamu. Lakini wakati alipounyosha mwili wake mdogo mnyonge, na kusema, ‘Lazaro, njoo huku,’ na mtu ambaye alikuwa amekufa kwa muda wa siku nne, akasimama kwa miguu yake. Hilo lilihitaji zaidi ya mwanadamu, huyo alikuwa Mungu katika Mtu huyo.” Ni nani anayeweza kuwafufua wafu, ila Mungu? Yeye Ndiye ufufuo na Uzima! Hiyo ni kweli.

⁸⁴ Usiku ule ule nje baharini, wakati alipokuwa kule, amechoka, amelala nyuma ya boti, ambapo pepo kumi elfu waliapa kwamba wangemzamisha usiku huo, na huo mtumbwi mdogo ukiwayawaya kama kizibo cha chupa huko nje kwenye bahari yenye tufani. Hao pepo waliwazia, “Tumempata sasa. Amelala; tualizamisha kundi hilo lote.” Loo, Yeye alikuwa Mwanadamu, amechoka, bali mara moja wakati alipoamka, aliweka mguu Wake kwenye demani, akaangalia juu na kusema, “Amani, tulia,” ndipo upepo na mawimbi vikamtii. Huyu alikuwa ni zaidi ya mwanadamu.

⁸⁵ Yeye alikuwa mwanadamu wakati alipokuwa na njaa. Alishuka kutoka mlimani, akitafuta kipande cha mkate ama kitu fulani cha kula, ama tini kutoka kwenye mtini. Lakini wakati alipochukua biskuti tano na samaki wawili, na kuwalisha elfu tano, huyo alikuwa ni Mungu katika Mtu yule. Hiyo ni kweli.

⁸⁶ Loo, kila mtu ambaye alipata kuwa si kitu chochote kile aliamini jambo hilo, washairi wote ambao waliamini jambo hilo. Si ajabu mmoja aliandika:

Alipoishi alinipenda; na alipokufa, aliniokoa;
Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
Alipofufuka, alinihesabia haki milele;
Siku moja Yeye anakuja, Ee siku ya utukufu!

⁸⁷ Eddie Perronet, wakati nyimbo zake zisingenunuliwa. Siku moja, akiyumbayumba chini ya nguvu za Roho Mtakatifu, alinyakua kalamu, akaandika ule wimbo wa kutunukia, wakati alipoandika:

Wote na wazisifie nguvu za Jina la Yesu!
Malaika na wamsujudi;
Leteni taji ya kifalme,
Mvikeni taji Bwana wa wote!

⁸⁸ Haleluya! Hakika, hivyo ndivyo tunavyoamini Yeye alikuwa. Naam, bwana.

⁸⁹ Yeye hana budi kuamini yasiyowezezana sasa, kwa mawazo ya kisasa ya siku hiyo. Vivyo hivyo inakubidi wewe kuamini kwa ajili ya yasiyowezezana, upate kuona Uzima mpya, kuona jambo fulani likitukia. Bali kama Yeye alitambua . . . Yeye alimtambua kuwa ni Neno, basi yasiyowezezana yanaweza kutukia, kwa sababu Yeye ni muumba, naye atatimiza kila kitu alichosema.

⁹⁰ “Na mambo yote yanawezekana kwa hao wanaoweza kuamini.” Hilo ni Neno Lake. Lakini yasiyowezezana yanadhihirishwa wakati Mungu anapochukuliwa kwenye Neno Lake. Naam, bwana. Wakati Mungu anapochukuliwa kwenye Neno Lake, yasiyowezezana yana—yanadhihirishwa. Wakati Mungu anaposema itakuwa, basi unachukua Neno hilo na uangalie yale, yasiyowezezana yakitukia. Bila shaka yatatukia.

⁹¹ Lakini angalia, hata katika hayo yote, yeye alisema, “Hata sasa, Bwana, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atalifanya.” Yeye alijua ya kwamba angaliweza tu kupata hilo Neno kutoka Kwake. Hilo tu ndilo alilohitaji kufanya, ilikuwa ni kulipata hilo Neno. Naam, ilikuwa ndiyo saa yake yenye giza sana, ndipo Yesu alikuja na akaita. Loo, ni jambo la jinsi gani waliloona, ufufuo!

Hebu na tuangalie wengine zaidi ambapo saa zenye giza sana zilikuja.

⁹² Kulikuwa na mtu mmoja wakati mmoja, jina lake Ayubu, mmoja wa manabii wa kale kabisa katika Biblia. Yeye alikuwa ni mtu mashuhuri. Alikuwa—alikuwa amempenda Bwana, na alikuwa amefanya yote aliyojua jinsi ya kufanya. Naye shetani alitaka kumpepete, kwa hiyo akamwambia Mungu siku moja. . . Naam, Mungu alimwambia, hasa, “Umetoka wapi, Shetani?”

⁹³ Akasema, “Loo, kuzunguka-zunguka huku na huko na hapa na pale duniani.”

⁹⁴ Akasema, “Je! umemwangalia huyo mtumishi wangu Ayubu?” Hapana mmoja aliye kama yeye duniani. Yeye ni mtu mkamilifu.”

⁹⁵ “Loo,” akasema, “hakika. Wewe unampa kila kitu, unamfanyia kila kitu. Hakika, yeye ni mtu mashuhuri. Lakini hebu niachie huyo wakati mmoja, nitaubadilisha msimamo wake. Nitamfanya akukufuru, mbele za uso Wako.”

⁹⁶ Akasema, “Huwezi.” Hiyo ni imani Yake katika mwaminio. Kwa nini? Yeye hana Kikomo. Yeye ni wa Milele. Anajua mwisho kutoka mwanzo. Alijua Shetani asingeweza kufanya jambo hilo. Kwa kuwa, Yeye ni Neno, alijua yale Ayubu angefanya.

⁹⁷ Sasa, kumbukeni, Ayubu, alimpiga kwa majipu, akawaua watoto wake, akatwaa yote aliyokuwa nayo. Afya yake ilikuwa imekwisha. Hata wafariji wake wakaja, nao wasingeweza kufanya kitu ila kumshtaki kwamba ni mtenda dhambi wa kisiri. Ndipo maskini Ayubu akafikia mahali fulani mpaka akadhikika sana.

⁹⁸ Inakubidi kudhikika, kwanza. Inakubidi kufikia wakati ambapo mambo yamefikia mwisho wake.

⁹⁹ Ayubu alifikia mwisho wa mambo, wakati aliposema, “Ilaaniwe siku niliyojaliwa. Jua hata na lisiangaze, wala mwezi usiangaze usiku, na hilo jina lisiitwe kamwe.” Na katika dhiki hiyo, ndipo Yesu alikuja. Aliangalia chini, na akasema, “Ninamwona mtu. Ua hufa, nalo linafufuka tena katika majira ya kuchipua. Mti ukianguka chini, unafufuka tena kwa harufu ya maji.” Aliona uhai wote wa mimea ukiishi tena, bali alisema, “Mwanadamu hulala mauti, anatoa roho yake, yeye yuko wapi?” Ulijua yeye alikuwa mzee. Alisema, “Wanawe huja kuomboleza juu yake, wala yeye hajui. Loo, laiti ungalinificha katika kaburi na kuniweka katika mahali pa siri, mpaka gadhabu Yako

itakapopita. Niwekee wakati na unipimie wakati. Tulienda . . .” Na akaendelea hivyo, akiongea. Alikuwa amefikia mwisho, wa dhiki yake, “Nini kingetukia? Majani huishi, yanarudi mtini, maua yanarudi tena, kila kitu kinajitokeza, bali mwanadamu hulala mauti na kutoa roho yake!” Alikuwa katika dhiki. Hakujua jambo ambalo lingeweza kumpata, naye akiwa kwenye umri huo.

¹⁰⁰ Wakati alipofanya hivyo, ndipo Yesu alipomjia. Mungu alikielekeza kichwa chake mbinguni, naye akamwona Yesu akiya katika siku za mwisho.

¹⁰¹ Hiyo saa yenye giza sana wakati mke wake aliposema, “Mlaani Mungu upate kufa mauti,” hata hivyo alisema, “Mwanamke, unanena kama mwanamke mpumbavu. Bwana alitoa, na Bwana ametwaa, jina la Bwana libarikiwe.” Hata mke wake alimkataa. Kanisa lake lilimkataa. Kila mtu alimkataa.

¹⁰² Katika ile saa yenye giza, ambapo hakujua mahali alikokuwa akienda kutoka hapo, Yesu alimjia. Ndipo akapaza sauti, “Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Na mabuu ya ngozi yajapouharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu, Ambaye nitamwona mimi mwenyewe.” Katika ile saa yenye giza totoro, ndipo Yesu akaja. Naam, bwana.

¹⁰³ Musa, kwa Musa, ile saa yenye giza sana ilimjia katika Israeli. Alikuwa katika wajibu wake; akakutana na Mungu katika kijiti, na kusema, “MIMI NIKO AMBAYE NIKO.” Alishuka akaenda na kupigana na kila namna ya uigaji wa Yane na Yambre, wakijaribu kuiga kazi yake. Yote haya, alikuwa amedumu mwaminifu kwa Mungu. Hatimaye aliwafanya Israeli kuamini. Naye huyu hapa anatoka Misri, akienda kwenye—kwenye nchi ya ahadi, ambako Mungu alisema, “Mtianiabudu kwenye mlima huu.” Hilo lilikuwa ni Neno la Mungu. Musa alijua ilimbidi kwenda kwenye mlima ule. Amina. Mungu alisema jambo hilo! Hakuna Farao anayeweza kumwua. Hakuna Ibilisi anayeweza kumwua. Hakuna kitu kinachoweza kumwua. Yeye anakuja kwenye mlima huo. Amina! Haleluya! Ninajisikia wa kidini. Yeye anaenda kwenye mlima huo.

¹⁰⁴ Vivyo hivyo tumo njiani kuelekea Utukufuni! Hakuna kitu kitakachotukomesha. La, bwana. Mungu atalithibitisha Neno Lake. Sijali ni kitu gani kitakachotukia, Yeye atafanya jambo hilo, hata hivyo.

¹⁰⁵ Yeye yuko njiani, katika wajibu wake. Huyu hapa, amezingirwa katikati ya milima. Anasikiliza na kusikia mngurumo nyuma yake. Ni kitu gani? Magari ya farasi za Farao, kwa maelfu, yakija; yenye silaha, na mikuki na kadhalika, kuwabwaga chini kwa farasi na kuwakanyaga chini. Ile pale Bahari ya Shamu, ilikuwa imewazuia. Yeye alifanya nini? Aliingia katika dhi...Aliingia katika dhiki. Watu wote

wakipiga makelele, “Loo, tutajuta sasa. Farao atatuua, mikuki yake itatuchoma. Watoto wetu wachanga watafia hapa nyikani.”

Musa akalia, “Ee Mungu!”

¹⁰⁶ Na ndipo Yesu akajitokeza jukwaani. Yeye alikuwa ile Nguzo ya Moto. Hilo ni kweli. Yeye alishuka na akaning’inia kati yake na hatari. Amina. Yeye ndiye mtetezi wetu. Yeye ndiye mtenganishaji, amina, mpatanishi. Huyu hapo alisimama, amesimama pale; giza kwa Wamisri, wale waliokuwa wakija kujaribu kufanya jambo fulani juu yake. Alikuwa nuru kwao, ya kusafiria. Ndipo asubuhi wakati upepo ulipoanza kuvuma kwa nguvu, usiku huo, basi Yeye alifanya nini? Alikuwa amekuja katika mfano wa Nguzo ya Moto.

¹⁰⁷ Kumbukeni, Yeye angali ndiye ile Nguzo ya Moto. Naam, bwana. Wakati alipokuwa duniani, Yeye alisema, “Nilitoka kwa Mungu, Na ninakwenda kwa Mungu.”

¹⁰⁸ Na baada ya mauti Yake, kuzikwa, kufufuka, na kupaa; Mtakatifu Paulo, akienda zake Dameski, alipigwa akaangushwa chini na ile Nguzo ya Moto. Kumbukeni, yeye alikuwa Mwebrania. Asingalisema jambo hili. . . Yeye alisema, “Bwana, U nani Wewe?” Herufi kubwa B-w-a-n-a, Elohimu. “U nani Wewe ninayemtesa?”

Akasema, “Mimi ni Yesu.”

¹⁰⁹ Amina! Haleluya! Yeye ni wa Kwanza na wa Mwisho. Yeye ni kila kitu. “Bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena, hata hivyo ninyi mtaniona. Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu.” Nguzo ile ile ya Moto, Mungu yeye yule akifanya jambo lile lile, kwa ahadi ile ile, amina, akilidhihirisha Neno Lake. “Mimi ni huo Ufufuo na Uzima. Mimi Ndiye niliyekuwako, Yeye Aliyeko, na Yeye Atakayekuja.” Ndio, bwana. Naam.

“Baba zetu walikula mana nyikani.”

¹¹⁰ Yeye akasema, “Wao, kila mmoja wao, amekufa. Lakini, MIMI NIKO AMBAYE NIKO.” Musa. . . Katika kijiti kilichowaka moto, huyo alikuwa ndiye MIMI NIKO. Yeye angali ni MIMI NIKO, si nilikuwa; MIMI NIKO, wakati uliopo, wakati wote.

¹¹¹ Tunaona hapa ya kwamba Musa amesukumwa pembeni, Naye Kristo alikuwa ameshuka. Sasa, na Biblia ilisema ya kwamba, ya kwamba, “Musa alihesabu ku—kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri.” Kushutumiwa kwake Kristo! Kristo alikuwa ni ule upako, yule Logos aliyetoka kwa Mungu. Yule Malaika, msomaji yeyote wa Biblia anajua ya kwamba yule Malaika alikuwa ni Kristo. Na alikuwa ndiye yule aliyekuwaka kule jangwani, Naye akajitokeza jukwaani, katika umbo alilopaswa kujidhihirisha ndani yake. Utukufu kwa Mungu!

¹¹² Yeye anakuja leo katika umbo, Kristo yeye yule, akimdhahirisha Yeye.

¹¹³ Yeye aliwaambia ya kwamba angewatoa. Alikuwa akifanya jambo hilo. Huyu hapo akaja kulitetea Neno Lake, kulithibitisha. Ndipo baada ya Yeye kuja, kama alivyofanya kwa Martha, ndipo aliita. Akasema, “Musa, kwa nini unanililia mimi? Nena na watu hawa, kwamba wasonge mbele.” Ile saa yenye giza, Bahari ya Shamu ikafunguka nao wakavuka, katika safari yao kulitimiza Neno la Mungu. Naam, kwenye saa ya Musa yenye giza nene sana, ndipo Yesu akaja. Tuna wakati sasa... Naye akamwita Musa.

¹¹⁴ Tunataka kuelekeza usikivu wenu kwa mtu mwingine mdogo. Jina lake lilikuwa ni Yairo. Wako wengi sana wa hao ulimwenguni leo. Yeye alikuwa mwamini wa siri. Alimpenda Yesu. Alikuwa amesikia habari Zake. Alimwamini. Lakini, unaona, alikuwa tayari amejiunga na madhehebu. Naam. A—a—alininii tu...Asingeweza kujitokeza na kukiri jambo hilo. Aliliamini, bali asingeweza kulikiri, kwa hiyo alikuwa amejiunga na wasioamini. Lakini kusema kweli aliamini.

¹¹⁵ Unajua, wakati mtu anapoingia katika hali hiyo, wakati fulani Mungu humleta kwenye shindano la kuamua. Ni katika dhiki ambapo kweli tunaonyesha vile tulivyo hasa, kile tulicho hasa.

¹¹⁶ Kwa hiyo huyo hapo, alikuwa tayari amejiunga na wasioamini, na alikuwa tayari ameenda kule na kuandika jina lake katika kitabu, na kadhalika. Naye alikuwa ni kuhani, na kwa hiyo ilikuwa ni vigumu kwa—kwake kukiri, maana hiyo ilikuwa ndiyo riziki yake. Kwa hiyo, lakini bado alimwamini Yesu.

¹¹⁷ Siku moja, maskini msichana wake alikuwa mgonjwa. Loo, jamani. Yeye, hapana shaka mtu huyo alikuwa amechukua, namna hiyo, angalimwita daktari. Tabibu alikuja, akamuuguza mtoto huyo. Homa ikazidi kuwa mbaya zaidi. Baada ya kitambo kidogo akawa na joto sana, na kila kitu, hatimaye akawa karibu na kufa. Alikuwa katika dhiki. Ilimbidi afanye jambo fulani. Yeye, kamwe hakujua la kufanya. Sasa yeye aliwazia, “Laiti ningaliweza kumpata, popote alipo.” Sasa hakungojea mpaka ilipofika wakati wa usiku, kama Nikodemo alivyofanya, apate mazungumzo ya faragha. Wakati uliwadia afanye kitu, wakati wa matendo ulikuwa umewadia naye hana budi basi kushughulika.

¹¹⁸ Nami nawazia, ndugu, dada, ndivyo ilivyo sasa. Wakati wa matendo umewadia. Wakati wa kuamini ama kutokuamini umewadia. Mstari huo wa kutengana humjia kila mwanamume na mwanamke. Humjia kila mtoto. Mara nyingine wakati unapovuka mstari huo, kuna jambo moja tu lililosalia, hilo

ni hukumu, wakati unapopita kati ya rehema na hukumu, unapovuka mstari huo.

¹¹⁹ Kumbukeni, aliingia katika kudhikika. Hakujua la kufanya. Wale pale makuhani wake wamesimama, waalimu wote wakisimama karibu naye. Unachama ulikuwa umemzunguka, watu wote kule jirani, wakimwalia msichana wake mdogo akifa. Daktari akisimama huko nje, amekunja mikono yake, akitikisa mikono yake, “Nimempa kila dawa niliyojua, na angali...”

¹²⁰ Unaona, ilikuwa ni Yesu akifanya kazi wakati wote. Yesu alikuwa akifanya jambo hili kwa kusudi fulani, kumwanika alivyo hasa maskini jamaa huyo. Baada ya kitambo kidogo, ninaweza kumwona akienda kuchukua kofia yake ndogo nyeusi na kuivaa, akavaa koti lake dogo la kuhani.

“Unakwenda wapi?”

¹²¹ “Nilisikia Yeye yuko huko chini mtoni. Ninakwenda kumtafuta!” Loo, jamani! Huyoo akaenda zake!

¹²² Katika saa hiyo ya dhiki, ilimbidi kufanya maamuzi: amwache mtoto wake afe, ama amtambue huyo alikuwa Ndiye dhihirisho la Neno. Alikuwa kuhani, naye alikuwa amelisoma Neno, naye alijua ya kwamba huyo alikuwa ndiye dhihirisho la Mungu. Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Yeye alijua jambo hilo, naye alilazimishwa kwenye jambo hilo. Ilimbidi kufanya kosa, amwache mtoto wake afe, vinginevyo akiri. Wakati alipoingia katika dhiki hiyo, ilikuwa ni karibu na wakati huo ambapo Yesu alikuja. Alikwenda kumwona. Akasema, akasema, “Nitakwenda na Wewe, lolote utakalosema.” Akiwa yuko nje barabarani, huyu hapa mjumbe anakuja, hiyo hapo balaa. Alikuwa amekiri, ya kwamba alimwamini Yeye. Alikuwa tayari basi amekwisha kujiondoa kwenye madhehebu yao, na kujionyesha hadharani wakati huo, ya kwamba alikuwa anamwamini Yesu.

¹²³ Basi huyu hapa mjumbe akija mbio, kasema, “Usimsumbue mtu yeyote, maana msichana wako amekufa tayari. Alikufa jana. Tayari amekufa. Usininii, usijipumbaze na jambo hilo tena.”

¹²⁴ Na, loo, maskini moyo wake karibu ukome kudunda. Bali aliangalia na kuona hayo macho ya Yesu, kasema, “Hivi sikukwambia? Usiogope, kama ukitaka kuona utukufu wa Mungu. Unahofu nini? Tayari nimekwambia ya kwamba ningeenda.”

¹²⁵ Yeye tayari amesema angekuja. Tayari amesema angefanya jambo hili, naye huyu hapa analifanya. Amina. Alisema angejitokeza jukwaani katika siku za mwisho na kufanya mambo haya kama alivyofanya, kama tulivyosoma jana usiku na kuyazungumza. Huyu hapa akifanya jambo hilo. Unahofu nini?

¹²⁶ Kumbukeni, wakati Yeye alipokuja, na akamwita kutoka kwa wafu. Alijitokeza jukwaani na akamfufua kutoka kwa wafu.

Maskini Batimayo kipofu, wakati mmoja, alifikia kwenye saa yake yenye giza nene sana.

¹²⁷ Yesu alikuwa mahali fulani huko, wakashughulikia kiamshakinywa cha Wafanyabiashara wa Full Gospel sehemu fulani kule—kule Yeriko, naye alikuwa na Zakayo kule. Alikuwa amekutana naye akiwa juu ya mti, huko chini barabarani. Kwa hiyo wakati alipokuwa... Vema, asingeshughulikia kitu kingine chochote, nina hakika. Unaona? Kwa hiyo basi wakati aliposhuka akaja kule, Yeye—Yeye alikuwa naye, Zakayo alikuwa ameambatana Naye.

¹²⁸ Maskini Batimayo kipofu alikuwa kipofu tangu alipokuwa mvulana mdogo. Kwa hiyo alifikiria huenda Yesu atatokea kwenye lango hilo, naye alikuwa akingojea. Baada ya kitambo kidogo alisikia kelele nyingi, na kila mtu akipita.

¹²⁹ Ndipo akamsikia kuhani akisema, “We! We, Wewe, Wewe unayekwea mlima pale! Je—Je—Je!... Tunasikia ya kwamba unawafufua wafu. Tuna uwanja mzima uliojaa hao kule juu. Kama Wewe ni Masihi, kama Wewe ni Masihi, njoo huku juu ukawafufue hawa wafu.”

¹³⁰ Unajua, ibilisi yuyo huyo angali anaishi, unaona, katika umbo la dini, kwa namna ile ile. Unaona?

¹³¹ “Kama Wewe ni Masihi, sisi... Wewe unafufua wafu; tuna uwanja wa makaburi uliojaa hao huku juu, Njoo.” Na, loo, kila mtu akipiga makelele. Mtu mmoja akipiga makelele, “Hosana kwa Nabii!” Mwingine akipiga makelele *hivi, vile*, ama *vinginevyo*. Mchafuko mtupu!

¹³² Maskini mwanamume huyu kipofu aliwazia, “Loo, nilimkosa. Alitokea kule chini, nami nilidhani angekuja hapa. Nimewekwa mahali pasipo.” Ndipo akaanza kupiga makelele. Akawazia, “Kama Yeye ni Neno, Yeye ni Mungu; hana budi kuwa.” Kwa hiyo, “Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!” Katika saa hiyo ya dhiki, yeye aliita.

¹³³ Sasa Yesu, kama utaliangalia hapa, alikuwa huko Yeriko. Ambako walisema alikuwa ameketi, alikuwa umbali wa yadi mia moja na hamsini kutoka mahali Yesu alipokuwa. Huku maelfu ya watu yakimkimbia huku na huko kumzunguka, asingeweza kusikia kilio cha mtu huyo. La. Bali alikihisi. Akasimama.

¹³⁴ Ninataka kuhubiri, moja ya siku hizi usiku: “Na ndipo Yesu akasimama.” Loo! “Na ndipo Yesu akasimama.” Loo!

¹³⁵ Lakini wakati Yesu aliposimama, ilikuwa ni kitu gani? Yeye alimwita. “Bwana amekuja. Usikate tamaa,” walimwambia wale wanafunzi, “Anakuita. Yeye anakuita.” Alimwita kutoka katika umati huo.

Yeye anafanya jambo lile lile sasa. Je! linakolea? Unaona?

¹³⁶ “Bwana amekuja na amekuita.” Naye anakuita utoke—utoke katika upofu uingie kwenye nuru, kutoka gizani kuingia nuruni. Naye akamwita, akapita kutoka mautini kuingia Uzimani. “Bwana amekuja na anakuita.” Na alipomwita, alimrudishia kuona kwake.

¹³⁷ Maskini yule mwanamke mwenye kutokwa na damu, wakati mmoja, huko juu kilimani, alikuwa ametumia pesa zake zote, kwa madaktari. Hapana shaka yeye alikuwa ameza fa—farasi wake wa vigari. Walikuwa wameza sha—shamba, wakaliweka rehani. Walikuwa wametumia yote waliyoweza kwa madaktari, hakuna hata mmoja wao aliyeweza kumsaidia. Aliendelea kuwa na hali mbaya zaidi na zaidi. Damu isingekoma. Daima, ilizidi kuendelea, akaugua zaidi na zaidi.

¹³⁸ Ndipo siku moja, alipokuwa ameketi pale akifuma, huko kilimani kutoka mahali alipoishi, aliangalia chini bondeni, naye akaona mtumbwi ukiingia. Kila mtu akaanza kukimbia, “Hosana kwa Nabii!”

¹³⁹ Alikuwa amesikia habari Zake. Imani chanzo chake ni kusikia. Sasa akasema, “Nitashuka niende nikamwangelie.”

¹⁴⁰ Ndipo wakati aliposhuka akaenda kule chini, na kwa mara ya kwanza akaona Neno la Mungu lililodhihirishwa katika mwili, kulikuwa na kitu fulani kuhusu mazungumzo Yake na jinsi alivyoonekana, hata akajua ya kwamba huyo alikuwa ni Yeye. Naam, bwana. “Loo, laiti ningaliweza kumfanya aniangelie kwa njia fulani, laiti ningaliweza kumgusa kwa njia fulani!” Ndipo akajipenyeza kwenye huo umati na akagusa vazi Lake.

¹⁴¹ Sasa kumbuka, Yeye hakuhisi kidole chake. La, bwana, kwa sababu vazi la Wapalestina linapwaya. Naye. . .

Ndipo Petro akasema, “Kila mtu amekugusa.”

¹⁴² Yeye akasema, “Lakini huu ni mguso wa tofauti. Naona nimekuwa mdhaifu.”

¹⁴³ Yesu alikuwa amekuja. Pesa zake zilikuwa zimekwisha, kila kitu kilikuwa kimekwisha; bali katika hiyo saa yenye giza ambapo damu isingekoma, wala madaktari wasingeweza kuizuia, Yesu alikuja. Naye alifanya nini? Alimwita. Akaangalia kila mahali mpaka akampata, Naye akasema, “Ulikuwa ukitokwa na damu, bali imekoma.”

¹⁴⁴ “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” “Bwana amekuja Naye anakuita. Amekuja na akaita.” Alimwita apate kuwa mzima tena.

¹⁴⁵ Maskini yule mwanamke kisimani, tuliyenena habari zake jana usiku, matumaini yote yalikuwa yamekwisha. Labda, huenda ikawa mume wake wa tano alikuwa amemwacha, naye ndio kwanza ampate wa sita usiku huo, naye—yeye alikuwa

anamshuku kidogo. Kiuadilifu, alikuwa amekwisha. Alitamani kuwa mama halisi wa heshima; yeye, hapana shaka, alikuwa akisoma Biblia.

¹⁴⁶ Naye alikuwa akielekea mahali pale, akipanda kwenda kule yapata saa tano. Asingeweza kuja asubuhi na mapema wakati wanawake waadilifu wanapokuja. Nao walibeba maji yao kichwani mwao, na majagi, wakashuka wakarudi. Na kwa hiyo asingeweza kuja, kuchanganyikana nao. Wao, walikuwa na ubaguzi wa jambo hilo siku hizo, waadilifu na wenye tabia mbaya hawakuchanganyikana. Watovu wa uadilifu walikaa mahali pao, kwa hiyo yeye asingeweza kuja pamoja na hao wengine. Wasingemruhusu kuja. Kwa hiyo baada ya kila mtu kuchota maji yao na kurudi. . . Yeye alikuja kwa ajili ya yaliyo Bora zaidi.

¹⁴⁷ Na ndipo akapanda akaja pale akiwa na nyungu hii kichwani mwake, hapana shaka alikuwa akienda zake, akiwazia, “Sasa, yule mwanamume niliyeolewa naye, niliyempata jana usiku, nina shaka naye. Yeye ni mwanamume, ni wa ajabu sana. Kabisa si—simwelewi. Sina bahati. Nimetupwa na jamii. Wala siwezi kwenda kwenye makanisa hayo, hawaninii. . . Hebu yaangalie tu! Sijui nifanye nini. Niko kwenye dhiki. Nami nimekuwa nikisoma Biblia; hakika, siku moja, huyo Nabii atajitokeza jukwaani. Sasa ninajua wao wamedai ya kwamba hakuna kitu kama hicho, na, ‘jambo hili litatukia labda miaka mia moja ijayo, na liko umbali wa miaka elfu moja. Tumekuwa tukilitazamia kwa maelfu ya miaka, wala halijatukia bado, kwa hiyo hatulitazamii sasa. Kila kitu ndivyo kilivyo. Loo, la, tuna makanisa na kadhalika. Hatuhitaji kitu chochote kama hicho sasa.” Kwa hiyo basi alikuwa akienda zake namna hiyo pale, akiwazia.

¹⁴⁸ Unajua, unapowazia habari Zake, hapo ndipo Yeye anapokutokea. Kama vile tulivyosema jana usiku, wakati walipokuwa wakienda zao Emau.

¹⁴⁹ Wakati mama huyo alipowazia mambo hayo, alimsikia Mwanamume mmoja akisema, “Nipe maji ninywe.”

¹⁵⁰ Vipi kuhusu jambo hilo? Katika saa zake zenye giza sana, wakati uadilifu wake ulikuwa umekwisha. Labda ni maskini mama mmoja mrembo, alikuwa ametupwa mitaani kuishi namna hiyo. Mara nyingi si kosa la maskini msichana huyo, ni kosa la wazazi wake, kumwacha atoke nje namna hiyo. Naye huyo hapo, labda maskini nywele zake za mawimbiwimbi zote zikining’inia chini; alikuwa amekaribia kwisha kabisa, akisukuma maisha, amechoka, wala hakuna mtu aliyekuwa akijihusisha naye, mtoto huyo, na labda ana hadithi nzito nyuma yake.

¹⁵¹ Hata hivyo, ninajua jambo moja, yeye alikuwa ameisoma Biblia, naye aliamini Biblia. Na kulikuwa na mbegu ndogo

ikikaa moyoni mwake, ikisema, “Kama litatukia wakati wowote, nitajua.” Alikuwa amekusudiwa kwa jambo hilo.

¹⁵² Hebu mwangalie maskini yule Yuda amesimama pale na akitenda jinsi alivyotenda. Ilikuwa ni giza kwenye kilindi cha moyo wake. Ile Nuru ilikuwa ikiangaza juu hapa katika matendo yake, bali moyoni mwake yeye hakuiamini. Naye huyo hapo yule mwanamke . . . Unaona, ile Nuru isingeweza kuingia kwenye kitu hicho. Lakini huyo hapo yule mwanamke, aliamini, aliliamini, bali maisha yake yalikuwa ni giza tupu; wakati ile Nuru ilipomulika, ililitoa nje hilo giza. Bali wakati hiyo Nuru ilipomulika hapa juu, ilipatia pote giza. Hiyo ndiyo tofauti yake.

¹⁵³ Unaona, alizaliwa kwa kusudi hilo. Yule mwanamke, yeye alisema, wakati Yeye alipomwambia kwamba alikuwa na wanaume wangapi, yeye . . . Ni kitu gani kilichotukia? Mara moja alishikwa na msisimko. Akaingia katika kudhikika. Akasema, “Bwana, ninaona kwamba Wewe u nabii. Ninajua ya kwamba wakati Masihi atakapokuja, Yeye atafanya mambo haya.”

¹⁵⁴ Ndipo akamwita. Ndipo akamwita. “Mimi Ndiye, Yeye anayesema nawe.” Alitambua jambo hilo kwa Neno la Mungu. Yeye alimwita kutoka kwenye dhambi zake, kumwingiza Uzimani. Na jina lake limo katika Biblia, naye ana Uzima usiopatikana na mauti leo.

¹⁵⁵ Yeye anaweza kukuita kwa njia hiyo hiyo, kwa sababu Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ninii . . .

¹⁵⁶ Naam, uadilifu wake ulikuwa umekwisha, bali hata hivyo alijua ya kwamba alikuwa na ule upambanuzi. Alijua ya kwamba huyo ilibidi awe Ndiye Masihi. Ndipo wakati Yesu aliposema, “Mimi Ndiye, Mimi Ndiye,” yeye alijua huyo alikuwa Ndiye.

¹⁵⁷ Wakati mmoja wanafunzi walikuwa huko wakisafiri katika mtumbwi, matumaini yote yalikuwa yamekwisha. Tufani, walikuwa wameondoka bila Yesu, na tufani zilikuwa tu—tu kama zilivyokuwa kwenye nyumba ya Lazaro. Matumaini yote yalikuwa yamekwisha. Ule mtumbwi mdogo ulikuwa umejaa maji. Nao walikuwa wakipiga mayowe na kulia, na labda wakiomba na hali hiyo ikiendelea, na radi ikimulika, na ule mtumbwi kujazwa na maji, nguzo za mlingoti zilianguka chini, makasia yalivunjika, nao walikuwa wameshikana, wakilia.

¹⁵⁸ Na katika saa hiyo yenye giza sana, ndipo Yesu aliwajia akitembea. Lakini alionekana kama kivuli kwao. Alionekana ni wa kutisha, kama roho fulani, nao wakapiga makelele kwa hofu.

¹⁵⁹ Hiyo ndiyo shida leo. Yesu huja katika saa ya saa yako ya giza, nawe unaogopa jambo Hilo. Hujui ni kitu gani.

¹⁶⁰ Hawakujua Yeye alikuwa ni kitu gani. Wakasema, “Loo, ni roho!” Walikuwa wakipiga makelele.

¹⁶¹ Na ndipo Yeye akawaita, kasema, “Msiogope, ni Mimi.” Katika saa yenye giza sana, Yesu akaja kule, msaada wao. Hivyo ndivyo anavyofanya daima, anakuja katika saa yenye giza kuliko zote. Ndipo Yesu akaja na kujidhihirisha Mwenyewe, na akawajia.

Petro akasema, “Ikiwa ni Wewe, niambie nije juu ya maji.”

Yesu akasema, “Njoo.”

¹⁶² Mnajua ni nini, wapendwa? Hivi karibuni Yeye atakuja kwa ajili ya hao katika siku hizi za mwisho. Sasa, si ni ajabu ya kwamba kanisa limeingia katika saa hii yenye giza tena?

¹⁶³ Nitasema jambo fulani hapa. Si fundisho. Ninatabiri tu. Mnajua ni jambo gani lililotukia? Itafikia mahali, hivi karibuni, lishikeni neno langu, ambapo itabidi madhehebu yote kujiunga na Baraza la Ekumeni. Wasipojiunga nalo, hawawezi kuungwa mkono na Baraza hilo. Kwa hiyo, kutakuwa na kususiwa, wala hakuna mtu anayeweza kwenda kwenye makanisa haya, ama kwenda kwenye makanisa yoyote; usipokuwa na alama kutoka kwenye kanisa lako mwenyewe, huwezi kununua wala kuza. Unalion tu kama vile lilivyokuwa, kwa hiyo litatukia tena, alama ya mnyama. Nalo kanisa, wanatambua jambo hilo, watu wa kiroho.

¹⁶⁴ Na ninyi Wapentekoste, hata hivyo, mnatambua jambo hilo. Mmeanza kulihisi. Wakati makanisa yenu, mengi ya madhehebu ya Kipentekoste; wala sina haja ya kuyataja majina yenu, bali mnajua sasa hivi wanafanya hivyo, wanaingia ndani ya kitu hicho. Tayari wameshuhudia ya kwamba waliingia. Na mtakapofanya jambo hilo, itawabidi kufanya nini? Itawabidi kupoteza mafundisho yenu ya Kiinjilisti ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Itawabidi kupoteza mafundisho yenu ya Biblia.

¹⁶⁵ Nao washiriki hawatavumilia jambo hilo. Wakristo halisi waliozaliwa mara ya pili watakufa, kwanza. Wamezaliwa kwa Neno. Wanajua jambo hili linakuja. Naam, bwana.

¹⁶⁶ Na hivi jambo hili si ni la ajabu? Na katikati ya saa hii yenye giza sana, ndipo Yesu anakuja na kuwaita, kasema, “Msiogope. Ni Mimi. Ningali niko pamoja nanyi. Niko hapa kuthibitisha Neno Langu.” Na kama vile alivyokuwa wakati huo, ndivyo alivyo na leo hii. Yeye alisema angefanya jambo hilo. Loo, jamani! Bwana amekuja na ametuita.

¹⁶⁷ Watu wengi wagonjwa hapa, hapana shaka, kwamba wameketi hapa, na daktari amekwambia hakuna—hakuna tumaini kwako. Huenda ukawa katika saa yako yenye giza sana, lakini, kumbuka, Bwana amekuja na akakuja.

¹⁶⁸ Na siku moja, siku moja, Bwana atakuja na kuita kila jina lililoandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Kama yenu hayamo mle, liandike mle sasa, kwa maana Yeye atakuja na kuita. Hata wale walio makaburini wataisikia Sauti

Yake na watafufuka katika Uzima. Bwana atakuja na kukuita. Na wakati anaita leo, jibu na ufanye matayarisho kwa ajili ya Siku hiyo, ndivyo ninavyokushauri.

¹⁶⁹ Ahadi ya wakati huu, Yeye aliahidi angekuwa hapa. Mambo aliyoyafanya, angeyafanya tena, na sasa tena Bwana amekuja na anakuita.

¹⁷⁰ Na tuinamishe vichwa vyetu. Nina kama kurasa zingine sita hapa, bali si—siwezi kuzifikia hizo sasa. Na tuinamishe vichwa vyetu. Niliahidi kuwaachilia mtoke mapema, na tayari robo saa imepita.

¹⁷¹ Baba wa Mbinguni, Ee Bwana, jalia litukie tena. Mambo yote hayo ambayo nimesema, “Yesu amekuja na anakuita.” Yeye hufanya nini hapo anapokuja? Huita. Na jalia litendeke tena, Bwana. Jalia Roho Wako Mtakatifu aje miongoni mwa watu usiku wa leo, Bwana Yesu katika umbo la—la Roho. Jalia aje usiku wa leo na ajifunue Mwenyewe, halafu ajidhihirishe Mwenyewe. Kama wale watu, jinsi walivyoamini, tutaamini, pia, Bwana. Wapo wengi hapa, labda, ambao hawajapata nafasi hii. Tunaomba ya kwamba utawapa nafasi hiyo tena usiku wa leo. Kwa kuwa tunaomba kwa ajili ya utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁷² Mambo ndiyo hayo, dada, bali nenda zako tu na hilo. Hilo ni sawa. Endelea moja kwa moja. Loo, kimya kabisa, kila mtu.

¹⁷³ Je! mnaamini ya kwamba Yeye amekuja? Amekuja. Je! Yeye angali anaita wakati akija? Sasa kama tu mtaamini. Kama tu mtaamini Neno la Mungu, Mungu atalitimiza.

¹⁷⁴ Sasa angalieni, sina wakati wa kuitisha mstari wa maombi hapa. Nitawaita usiku wa leo, huko mliko, Bwana akipenda. Bwana amekuja. Amekuja kutimiza Neno Lake katika siku ya mwisho. Na jinsi alivyokuwa wakati huo, ndivyo alivyo leo. Jinsi udhihirisho ama utambulisho Wake ulivyokuwa wakati huo, ndivyo ulivyo leo, kwa sababu Yeye angali ni Neno la Mungu. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Na Neno la Mungu ni tambuzi la mawazo, makusudi ya moyo. Na jinsi alivyofanya wakati huo, ndivyo Yeye anavyofanya daima. Yeye angali ni yeye yule. Kama angefanya jambo hilo sasa hivi, je! mngemwamini? Lingewafanya mumwamini?

¹⁷⁵ Ninyi watu huko nje sasa, hebu niangalie kwanza nione kama kuna mtu yeyote ninayemjua, anayeketi mahali popote hapa ndani, ambaye ninamjua.

¹⁷⁶ Wote walio karibu, *hapa* juu, wasionijua mimi, inueni mikono yenu; wanaojua ya kwamba mimi siwajui kabisa, nanyi ni wagonjwa, inueni mikono yenu. Nadhani, ni kila mtu. Vema, sasa, ninyi aminini. Aminini tu kwa moyo wenu wote. Msitilie shaka. Iweni na imani. Mwaminini Mungu.

¹⁷⁷ Nitawaomba mwe watulivu sana, ketini. Msisogee hapa na pale sasa, tafadhalini msisogee. Mnaona? Mnaona? Ninzi ni na—nafsi, mwili, na roho. Na roho yako... Na Roho Mtakatifu ni makini sana.

¹⁷⁸ Ni wangapi wanaokumbuka, miaka kadhaa iliyopita, ya kwamba Roho Mtakatifu, wakati nilipokuja hapa na kuwaambia? Wakati nilipowashika watu mkono, Yeye aliniambia utambuzi huu ungekuja, na halafu utaendelea? Mnakumbuka jambo hilo, mnalikumbuka hilo? Lakini alisema, “Kama unaweza kuwafanya watu wakuamini.” Je! mnakumbuka siku hizo, miaka mingi iliyopita? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hamna budi kuamini.

¹⁷⁹ Nilimwona mtu mmoja, nafikiri ilikuwa ni hapa chini kwenye ule mkutano mwingine, ameketi moja kwa moja pale. Na Roho Mtakatifu... Nimekuwa nikimwangalia wakati nilipokuwa nikihubiri. Alikuwa kiwete. Alikuwa anatembea na mikongojo. Na wakati tu nilipoanza kutoa wito, Shetani alimjia mtu huyo, kivuli cheusi. Nami nikiangalia kwa macho yangu mwenyewe. Aliamka, akatoka nje. Yeye daima atakuwa kiwete, unaona. Na kwa hiyo, yeye, ambapo angeponywa pale pale kama angalininii tu—kuninii tu... Unaona? Lakini, ninii tu, sijui ni kwa nini. Nadhani alimsikiliza tu adui. Lakini kama ungesimama na kuangalia vivuli hivyo, uone mambo hayo katika maumbo, jinsi yalivyo, na kuyaangalia jinsi yanavyofanya. Unaona, ingekuwa hivyo.

¹⁸⁰ Sasa, mimi siwezi kuponya. Mtu anayekwambia ya kwamba anaweza kukuponya, anakosea. Umeponywa tayari. Lakini, ni kutambua Uwepo wa Yesu Kristo. Sasa kama Martha alijua ya kwamba angeweza kumwona Yeye tena, kwamba angepata shauku yake, kwa maana Yeye alikuwa ndilo Neno lililodhihirishwa, hivi hatuwezi kuamini kiasi hicho usiku wa leo, kuamini jambo hilo? Hakika, tunapaswa kuamini. Yeye amekuja. Amekuja, amekuja katika mfano wa Roho Mtakatifu. Hivyo ndivyo Yeye alivyo. Sasa ninyi ombeni tu.

¹⁸¹ Sasa, hapa juu, kama ningelikuwa na mtu fulani amesimama hapa, papa hapa karibu na mimi, kuninii tu—kuomba tu; nimeona watu wengi sana wakiomba, ni kote jengoni. Inakupasa tu kuchunga jambo hilo. Huwezi kusema, “Aisee, Ndugu Branham...” La, bwana. Ni—nisingeweza kufanya jambo hilo, si zaidi ya vile unavyoweza kuniotea ndoto. Unaona? Huenda ukaota. Wewe, Mungu angeweza kukufanya uniotee ndoto, unaamini jambo hilo, bali huwezi kufanya jambo hilo wewe mwenyewe. Huwezi kusema, kwamba, “Ndugu Branham, nitaota ndoto juu yako sasa.” La, huwezi kufanya hivyo. Wala mimi siwezi kuona ono. Yeyote yule anayekupa ndoto, huyo ndiye anayepaswa kufanya jambo hilo. Ndivyo ilivyo na ono pia.

¹⁸² Ninamwona mtu fulani ameketi papa hapa mwishoni mwa safu, akiwa na yabisi kavu. Kama ataamini kwa moyo wake wote, Mungu atamponya hiyo yabisi kavu. Je! unaamini Yeye atafanya hivyo, bwana? Unayeketi hapo, Mmekisiko mwanamume, unayeketi mwishoni mwa safu hiyo, je! utaamini? Vema, bwana.

¹⁸³ Bibi anayeketi karibu na wewe, yeye pia ana yabisi kavu, pia. Je! unaamini Mungu atakuponya, bibi? (*Hii* ina mwangwi? Nasikitika watu hawasikii.) Utaamini? Vema.

¹⁸⁴ Vipi kuhusu maskini yule bibi Mmekisiko mwingine anayeketi karibu naye? Anaugua ugonjwa wa tumbo. Je, unaamini Mungu ataponya tumbo lako, mama?

¹⁸⁵ Ameupata. Ninapooni ile Nuru ikishuka chini, hilo linamaanisha limetukia. Naam. Jambo ndilo hilo. Ilimgusa. Hiyo hapo, ikizungukazunguka moja kwa moja. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . .hilo linatosha. Unaona? Anapoweza kupata imani! Unaona, “Asingeweza kufanya mambo mengi kwa sababu ya kutokuamini kwao.”

¹⁸⁶ Huyu hapa mama fulani ameketi hapa akiomba, papa hapa. Anahofu. Anapaswa kuhofu. Yeye ana ugonjwa wa kansa, mbaya sana. Sikujui mimi, bali Mungu anakujua. Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia juu ya kansa hii, ama kitu fulani chochote kile? Niangalie. Kuna wengi sana pale wanaoomba, unaona, hiyo ndiyo sababu ninasema hivyo. Tungalie. Sasa, naam, hutoki hapa, haya si makazi yako. Umetoka mahali panapoitwa Porterville, California. Hiyo ni kweli. Je! unaamini Mungu anaweza kuniambia kwamba wewe ni nani? Yeye anajua. Jina lako ni Bibi Wintham. Hiyo ni kweli. Sasa amini, na hiyo kansa itakuacha. Kama unaweza kuamini! Hivyo tu ndivyo Mungu anavyotaka kufanya. Kama unaweza kuamini!

¹⁸⁷ Hivi huamini jambo hilo kwa moyo wako wote? Mtu fulani upande huu *hapa* ndani, hivi huwezi kuamini? Bwana amekuja na kukuita. Anakuia kutoka mautini kuingia Uzimani, kutoka kwenye ugonjwa kuingia kwenye afya.

¹⁸⁸ Huyu hapa mtu anayeketi papa hapa nyuma, ameinamisha kichwa chake, akiomba. Kwa kweli yeye hajiombei, anaomba kuhusu mtu mwingine. Ni m—msichana. Ni binti yake. Je! unaamini, bwana? Una shida ya miguu yako. Una shida ya goti lako. Hiyo ni kweli. Hakuna haja ya kulia, Huyu ni Yeye hapo karibu na wewe. Binti yako yuko hospitalini, sivyo? Ugonjwa wa kifua kikuu. Wewe amini. Je! unaamini? Bwana amekuja na anamwita binti huyo. Je! utaamini ya kwamba utamkuta akiwa mzima kabisa? Utaamini? Na amtembelee usiku wa leo, na wewe. Na liishe.

¹⁸⁹ Huyu hapa maskini mvulana mdogo, maskini mvulana mdogo maji ya kunde. Ana ugonjwa wa ngozi, na pumu, mvulana

mdogo wa Kimeksiko, mvulana wa Kimeksiko anayeketi pale. Hatoki hapa. Ametoka San Jose. Je, unaamini, mwanangu? Jambo lingine, baba yako yupo hapa pamoja na wewe. Yeye ni mhudumu. Hiyo ni kweli. Je! unaamini Mungu anaweza kuniambia jina lako ni nani? Je! ingekufanya uamini sana? Jina lako ni Reubeni. Sasa amini. Vema.

¹⁹⁰ Bwana amekuja na anakuita. Loo, ewe mwenye dhambi, loo, ewe mgonjwa, hivi huoni Bwana aliyedhihirishwa katika mwanadamu, katikati ya waamini? Yeye amekuja kuwaita watoto Wake wanaoamini wapate afya. Amekuja kumwita mwenye dhambi apate kutubu. Ewe uliyerudi nyuma, mfuasi wa kanisa, Bwana amekuja na anakuita.

¹⁹¹ Je! unaamini jambo hilo? Je! unaamini jambo hilo ni kwa ajili ya haja yako sasa hivi? Kama unaamini, inua mkono wako, useme, “Ninaamini kwa ajili ya haja yangu.” Basi simama kwa miguu yako sasa na ulikubali. Bwana amekuja na anakuita. Na hata uwe ni nani, hata uwe una haja gani, Bwana amekuja Naye anakuita. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁹² Maskini mwanamke huyo aliingia mjini, na kusema, “Njoni, mtazame Mtu aliyeniambia nilikuwa na shida gani.” Wewe hukuingia mjini. Ulikuwa na kuona jambo hilo, wewe mwenyewe, kwa hiyo Bwana amekuja na anakuita.

¹⁹³ Inueni mikono yenu na mumsifu, na kusema, “Bwana Yesu, mimi ni mwenye dhambi; nisamehe. Mimi nimerudi nyuma; nirudishe, Bwana. Ninahitaji Roho Mtakatifu; nijaze. Mimi ni mgonjwa; niponye. Mimi ni kiwete; niponye.” Bwana amekuja na anakuita. Inua mikono yako sasa na umpe sifa. Amina.

¹⁹⁴ Tupe tuni kidogo hapa, “Nitamsifu, nitamsifu.” Mwajua, “Nitamsifu.” Mnaujua hu sivyo? Je! mnaamini?

Nitamsifu, nitamsifu,
Loo, nitamsifu Mwana-Kondoo aliyechinjwa
kwa ajili ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu, enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

¹⁹⁵ Je! mnampenda? Sasa hivi hampendi kumwambia wakati Yeye akiwa yupo hapa? Yeye ni Roho anayetembea hapa na pale humu jengoni. Yeye anajua mioyo yenu, anajua yote kukuhusu wewe. Hebu na tumwimbie, kwa moyo wetu wote.

Nitamsifu, (inua mikono yako unapofanya
jambo hilo), ni-...(sasa msifuni tu)...
tamsifu,
Loo, nitamsifu Mwana-Kondoo aliyechinjwa
kwa ajili ya wenye dhambi;
Loo, mpeni utukufu, enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

¹⁹⁶ Loo, mama, wewe uliye kwenye kiti cha magurudumu, laiti tu ungaliamini kidogo zaidi papo hapo. “Ni...” Hebu na tuujaribu mara nyingine tena. Ninangojea kitu fulani.

Nitamsifu, nitamsifu,
Loo, nitamsifu Mwana-Kondoo aliyechinjwa
kwa ajili ya wenye dhambi;
Mpeni sifa, enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

¹⁹⁷ Sasa wakati tukiuiimba huo tena, geukeni, ushike mkono wa mtu fulani, wakati tukiuiimba, tuimbe, “Nitamsifu.” Hima, sote pamoja sasa.

Nitamsifu, nitamsifu,
Nitamsifu Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi;
Mpeni sifa, enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

¹⁹⁸ Loo, rafiki mwenye dhambi, je! huwezi kutembea uje hapa sasa? Njoni huku na mumpe sifa, enyi watu wote. Ninyi nyote mnaotaka kumkiri kama Mwokozi. Katika Uwepo Wake, wakati watakatifu wanaabudu katika Roho, je! huwezi kuja hapa na kusimama? Useme, “Ninataka kushuhudia, usiku wa leo. Ninataka kumpa sifa. Ninataka kuja. Mimi simwonei aibu. Ninataka ulimwengu ujue ya kwamba ninamkubali kama Mwokozi wangu, papa hapa wakati akiwapo.” Njoo wakati tukiuiimba.

Nitamsifu, (je! huwezi kuja?) nitamsifu,
Loo, nitamsifu Mwana-Kondoo aliyechinjwa
kwa ajili ya wenye dhambi;
Loo, mpeni utukufu, enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

¹⁹⁹ Loo, namna hiyo, mama, njoo moja kwa moja. Ni nani mwingine atakayekuja, Mbele za Kristo? Njoo moja kwa moja huku, dada, simama hapa.

²⁰⁰ Mtu mwingine anayemtaka kwamba awe Mwokozi wako, sasa hivi, ambaye haoni aibu. Yeye alisema, “Ukinionea haya Mimi mbele za watu, nitakuonea haya mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu.” Kama humwonei haya sasa, na unamtaka awe Mwokozi wako, wakati akiwa hapa! Umemwona Yeye. Ni jambo kamilifu sana, Neno Mwenyewe kulifanya lijulikane. Njoo wakati watakatifu wanaabudu sasa. Hivi huwezi kuja?

²⁰¹ Mungu akubariki, bwana. Huyu hapa bibi mzee anakuja, akija kwenye umri wenyewe hasa. Hivi huwezi kuja sasa?

Nita-... (uimbeni sasa)... Nitamsifu...

²⁰² Hiyo ni kweli, enyi vijana, njoni moja kwa moja hapa. Msifuni tu. Mungu akubariki, bibi, hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo. Mungu awabariki, enyi vijana.

... aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu, enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

203 Wakati wahudumu wakiwaendea watu hawa sasa mtu mwingine si aje? Wewe uliyerudi nyuma, je! utakuja, useme, “Ninayaonea aibu maisha yangu”? Huyu hapa. Je! unaamini kwamba mimi ni mtumishi wa Mungu? Inua mikono yako. Mbona, Yesu Kristo yupo miongoni mwetu. Je! huwezi kuja?

Mpeni utukufu... (je! hamwezi kuja, mumphe utukufu?)... watu,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila...

204 Martha, je! unakuja, ama utaketi nyumbani pamoja na Mariamu? Je! utakaa huko nyuma kwenye madhehebu fulani, na kusema, “Loo, kanisa langu haliadini jambo hilo namna hii,” wakati Kristo amedhihirishwa? Je! utaketi kitako na kusema hivyo, ama unatoka? “Vema, nitakwambia, wakati mimi...” La. Leo, hii ndiyo ile saa. Mauti inaning’inia karibu nawe, kama binti wa Yairo.

205 Njoo sasa! Wewe uliyerudi nyuma, njoo sasa. Mwenye dhambi, njoo sasa. Huu ndio ule wakati. Bwana amekuja na anakuita. Yeye anakuita. Unasema, “Ninajuaje?” Yeye anatumia sauti yangu. Kama anatumia sauti yangu kuyatambua magonjwa, mateso na kadhalika, hivi hujui Yeye anaita pia kwa ajili ya dhambi. Toka! Njoo sasa, huenda hii ikawa ndiyo nafasi ya mwisho utakayopata kuwa nayo.

206 Mara nyingine tena, kuna wengine zaidi hapa ndani wanaopaswa kuja, enyi marafiki. Sitaki kuwatahayarisha, kuwaita namna hii. Hilo si sawa. Kama wakati mwingine labda utaninii... Hao Mafarisayo walidhani walikuwa wameokoka, lakini hawakuwa wameokoka. Mnafikiria jinsi ile ile. Njoni sasa.

207 Uwe na hakika! Usininii, usibahatishe tu nusunusu juu yake. Kama kuna tashwishi ndogo niani mwako, usibahatishe. Njoo sasa. Sasa ndio wakati wenyewe, sasa wakati ile Chemchemi imefunguliwa, wakati Roho Mtakatifu yupo hapa. Bwana amekuja. Hiyo tashwishi ndogo, ndiyo anayojaribu kukwambia, “Unatilia shaka.” Iondoe. Njoo, sasa. Bwana amekuja na anakuita. Naam, endeleeni tu kuja, endeleeni kuja moja kwa moja.

Nitamsifu, nitamsifu, (Je! huwezi kuja na kumpa sifa?)
Nitamsifu Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
Mpeni sifa, enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

²⁰⁸ Sasa wakati wenye dhambi wanakuja, kumdai Yeye; hebu watu na wampe sifa, tunapouimba sasa. Inueni mikono yenu, imbeni, na tumsifu, sote pamoja.

Nitamsifu, nitamsifu,
Nitamsifu Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi!

²⁰⁹ Mpeni tu sifa! Ninyi watu mlio karibu na hapa, ombeni, mwombeni awasamehe. Hivyo ndivyo atakavyofanya. Bwana amekuja na anakuita. Mungu awabariki.



NDIPO YESU AKAJA NA KUITA SWA64-0213
(Then Jesus Came And Called)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 13 Februari, 1964, kwenye Ukumbi wa Elliott huko Tulare, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2008 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org